JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA KUMI

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TISA

09 JFEBRUARI, 2018

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA TISA TAREHE 09 FEBRUARI, 2018

## I. DUA

Saa 3:00 asubuhi Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson alisoma na kuongoza Kikao cha Bunge.

**MAKATIBU MEZANI:**

1. Ndg. Stephen Kagaigai
2. Ndg. Ramadhani Abdallah
3. Ndg. Asia Minja
4. Ndg. Nenelwa M. Wankanga

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**1. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Taarifa ya Mwaka ya Upimaji na Utekelezaji wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma kwa Mwaka 2016/2017.

**2. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Mheshimiwa Yahaya Massare aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2016/2017.

**3. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Mhe. George Lubeleje aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa Mwaka 2017.

**4. MASWALI:**

Maswali yafuatayo yaliuzwa na kujibiwa

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Swali Na. 108 Mhe. Azza Hillary Hamad

Nyongeza
(i) Mhe. Azza Hillary Hamad
(ii) Mhe. Daimu Iddi Mpakate
(iii) Mhe. John Wegesa Heche
(iv) Mhe. Josephine J. Genzabuke

Swali Na. 109 Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King

Nyongeza
(i) Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King
(ii) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest
(iii) Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa
(v) Mhe. Mussa Azzan Zungu

Swali Na. 110 Mhe. Innocent Lugha Bashungwa

Nyongeza
(i) Mhe. Innocent Lugha Bashungwa
(ii) Mhe. Mwanne Ismail Mchemba
(iii) Mhe. Frank George Mwakajoka

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Swali Na. 111 Mhe. Abdallah Dadi Chikota

Nyongeza
(i) Mhe. Abdallah Dadi Chikota
(ii) Mhe. Khadija Nassir Ali

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Swali Na. 112 Mhe. Khalifa Mohammed Issa

Nyongeza Mhe. Khalifa Mohammed Issa

WIZARA YA AFAYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WAZEE NA WATOTO:

Swali Na. 113 Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma

Nyongeza (i) Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma
(ii) Mhe. Paschal Yohana Haonga

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na. 114 Mhe. Aida Joseph Khenan Kny. Mhe. Sophia H. Mwakagenda

Nyongeza (i) Mhe. Aida Joseph Khenan

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Swali Na. 115 Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa

Nyongeza (i) Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa
(ii) Mhe. Maryam Salum Msabaha
(iii) Mhe. Philipo Augustino Mulugo

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Swali Na. 116 Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

Nyongeza Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 117 Mhe. Ezekiel Magolyo Maige

Nyongeza (i) Mhe. Ezekiel Magolyo Maige
(ii) Mhe. Abdallah Ally Mtolea
(iii) Mhe. Stephen Hillary Ngonyani

WIZARA YA MADINI:

Swali Na. 118 Mhe. Ignas Aloyce Malocha

Nyongeza Mhe. Ignas Aloyce Malocha

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

Swali Na. 119 Mhe. Joyce Bita Sokombi

Nyongeza Mhe. Joyce Bita Sokombi

WIZARA YA NISHATI:

Swali Na. 120 Mhe. Omary Tebweta Mgumba

Nyongeza (i) Mhe. Omary Tebweta Mgumba
(ii) Mhe. Justine Joseph Monko

**MATANGAZO:**

i. Wageni mbalimbali waliokua Ukumbini walitambulishwa Bungeni;

**ii.** Wabunge walitangaziwa kuchukua nakala za Mwongozo wa Mawasiliano katika Pigeon holes;

iii. Naibu Spika alitoa majibu ya Mwongozo wa Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba Wabunge wakati wa uchangiaji wamekuwa wakivunja Kanuni ya 64(1) (d) kwa kutumia utendaji kazi wa Rais Kuhalalisha Hoja zao wakati mwingine kupotosha maana. Mfano ulitolewa ni uchangiaji wa Mhe. Abdallah Mtolea.

Kiti kilitoa mwongozo kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 45 imempa mamlaka Rais kusamehe mkosaji yeyote kwa kosa lolote, hivyo Mhe. Rais hajaenda kinyume na Katiba kama Mhe. Mtolea alivyokuwa akitaka kuliaminisha Bunge.

Na kwamba Mhe. Rais anawaalika wakosaji kufanya shoo habari hizo siyo za kweli kwa sababu Rais hajawahi kufanya hivyo. Hivyo hiyo ni dhihaka kwa Rais.

Hivyo kwa kutumia Kanuni ya 5 na 72 Kiti kinaagiza maneno yote yaliongelewa na Mheshimiwa Abdallah Mtolea yamekiuka kanuni hivyo yafutwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Aidha, Wabunge wote wanapochangia wahakikishe wanazingatia kanuni ya 64.

**MWONGOZO:**

i. Mheshimiwa Aida Joseph Khanan alitumia Kanuni ya 68(7) na 46(1) kuomba mwongozo kwamba majibu kwa maswali yake Na. 114 hayaridhishi na kiti kilielekeza kwamba majibu ya mwongozo atayatoa baada ya kujiridhisha na hansard;

ii. Mhe. Khatibu Haji alitumia Kanuni ya 64(1) kuhusu maswali yake kutojibiwa wakati wengine wanajibiwa na hakuna taarifa kutoka Ofisi ya Bunge. Kiti kilishauri aende idara inayohusika na maswali ili kupata majibu sahihi na kama hapati majibu aende Ofisi ya Spika.

iii. Mhe. Peter Simon Msigwa alitumia Kanuni ya 64(1) aliomba kuhusu utaratibu na alitaka kujua kazi ya Bunge na kwa nini Rais analindwa wakati Wabunge wanapomwongelea. Kiti

kilielekeza kwamba kanuni ya 64(1) ni Kanuni ya Utaratibu ambayo inatumika wakati kuna Mbunge anazungumza. Aliongoza kwamba Katiba Jamhuri ya Muungano wa Tanzabua Ibara 100 na 101 inaruhusu uhuru wa majadiliano una mipaka ni kifungu 64 ndicho kimewekwa ili kuona mipaka hiyo inafuatwa kwa hiyo kanuni hizo zifuatwe.

iv. Mhe. John Constantine Kanyasu alitumia Kanuni ya 68 (7) kwamba Wavuvi katika Ziwa Victoria hukamatwa wakikutwa na samaki tofauti na majibu ya awali ya Wizara. Kiti kilielekeza Wizara itafute majibu sahihi na imjibu Mheshimiwa Mbunge leo katika swali hili Wizara itoe.

v. Mh. Cecil Mwambe alitumia Kanuni ya 68(7) kuhusu changamoto ya wakulima wa korosho kuibiwa pesa zao katika kimtandao. Kiti kilielekeza kwamba Waziri wa Ulinzi afuatilie suala hilo ili kuwasaidia wananchi.

vi. Mhe. Hamidu Bobali alitumia Kanuni ya 64(7) kuomba mwongozo na alitaka ufafanuzi wa Serikali kuhusu Timu ya Yanga kutopewa uwanja wa nyumbani kwa ajili ya mazoezi wakati wageni wamepewa. Kiti kiliekeza Waziri aliangalie suala hilo.

vii. Mhe. Deo Sanga alitumia Kanuni ya 68 (7) kuhusu Wabunge kubeza Serikali kuwa haijafanya jambo lolote wakati imefanya mambo mengi. Kiti kilijibu kuwa inategemea nini macho ya mtu yatachagua kuona nini.

viii. Mhe. Mwita Getere alitumia Kanuni ya 64(7) alitaka ufafanuzi wa Serikali juu ya mgogoro unaendelea kati ya vijiji vitatu katika Jimbo lake na Serikali hichukui hatua. Kiti kilielekeza kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani alishughulikie suala hilo lakini na Waziri wa Ardhi na Maliasili washirikiane ili kumaliza mgogoro huo.

## III Hoja za Kamati

1. Mhe. Balozi Adadi Rajabu, Mwenyekiti wa Kamati na Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama aliwasilisha Taarifa ya Kamati yake kuhusu Shughuli za Kamati zilizotekelezwa kwa Mwaka 2017; na

2. Mhe. Almas Maige, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge waliwasilisha Taarifa ya Kamati yake kuhusu Shughuli za Kamati zilizotekelezwa kwa Mwaka 2017.

Baada ya Uwasilishaji huo, Uchangiaji wa Jumla ulianza na wafuatao walipata nafasi ya kuchangia.

1. Mhe. Katani Ahmad Katani
2. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka
3. Mhe. Christine Gabriel Ishengoma
4. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa
5. Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa
6. Mhe. Nape Moses Nnauye

Mawaziri wafuatao walichangia kwa kujibu baadhi ya Hoja

1. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angelina Mabula

2. Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Harrison Mwakembe.

3. Naibu Waziri wa TAMISEMI – Mhe. Josephat Sinkamba Kandege

4. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mhe. Mwigulu Lameki Nchemba

5. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Mhe. George Huruma Mkuchika.

6. Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi

Wenyeviti wa Kamati mbili ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge walihitimisha Hoja zao na kuwaomba Wabunge wapokee na kukubali Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa zao yawe Maazimio ya Bunge. Mwenyekiti aliwahoji Wabunge na Bunge liliridhia Taarifa za kamati hizo mbili ziwe Maazimio ya Bunge.

## IV Taarifa ya Katibu wa Bunge

Katibu wa Bunge alitoa Taarifa ya kumalizika shughuli zote zilizopangiwa kufanyika katika mkutano zimekamilika.

## V Hoja ya kuahirisha Bunge

i. Waziri wa Mkuu alitoa Hotuba ya kuahirisha Bunge na Hoja ya ya kuahirisha Bunge mpaka tarehe 3 Aprili, 2018.

ii. Naibu Spika alilihoji Bunge na Hoja hiyo iliafikiwa. Wimbo wa Taifa uliimbwa na Bunge liliahirisha mpaka tarehe 3 Aprili, 2018 saa 3.00 asubuhi.